

KARIBU KUJIUNGA NA CHEKECHEA

Mpito wa Chekechea kwa Familia za Wingilugha na za Kimataifa



Mtoto wako anaanza safari mpya ya elimu rasmi. Wakati watoto wanajiunga na chekechea, mpito huu unaweza kuwa mgumu kwa familia. Shule za Umma za Kaunti ya Jefferson (JCPS) zina [rasilimali](#) za kusaidia familia za wingilugha na za kimataifa zinapoanza chekechea.

Unaweza kuomba ukalimani unapozungumza na mfanyakazi wa JCPS.

Unaweza kutumia Kadi ya Nazungumza kukusaidia. Beba kadi hiyo na uwaonyeshe wafanyakazi wa shule. Unaweza kuchapisha kadi ya karatasi au kuipiga picha kwa kutumia kamera ya simu yako.



Unapoagiza ukalimani, mfanyakazi wa shule atakuunganisha na mkalimani kupitia simu au programu. Utahitajika kusubiri wakati mfanyakazi anafikia huduma za lugha.

Mipango

- Iwapo familia yako inazungumza lugha zingine nyumbani, huenda mtoto wako akastahiki kupokea huduma za Mwanafunzi wa Kiingereza. Unaweza omba tathmini kwa hadi miezi sita kabla ya kuanza chekechea. Piga simu kwa Idara ya [Kiingereza kama Lugha ya Pili \(ESL\)](#) kupitia 502-485-3623 ili upate usaidizi.
- Mtoto wako anaweza kuhudhuria Camp Ready4K. Mpango huu wa JCPS wa msimu wa joto husaidia familia na watoto kujiandaa kwa mpito hadi chekechea. Watoto wanaweza kujifunza stadi mpya, kushirikiana na watoto wengine, na kujaribu mazoea ya shule. Usajili hufunguliwa mwanzoni mwa msimu wa kuchipua. Ili kujifunza zaidi, piga simu kwa (502) 313-4357 au utume barua pepe kwa <mailto:jcps.help@jefferson.kyschools.us>.

Mahitaji ya Afya

Jimbo la Kentucky lina [mahitaji ya afya](#) kwa watoto wanaoanza shule. Mtoto wako atahitaji ukaguzi wa mwili na chanjo. Tembelea [Vituo vya Afya ya Familia](#) upate watoa huduma, huduma, na taarifa katika lugha unayopendelea.



Mahitaji ya Usajili

Ili kujiandikisha shuleni, unapaswa kuleta karatasi za kuonyesha ulezi na makazi **Familia zinaweza kusajili watoto wao licha ya hali ya uhamaji**



Aina ya Hati	Hati Inayokubalika
Uthibitisho wa Kuzaliwa kwa Mtoto	Cheti cha kuzaliwa, pasipoti, au fomu ya I-94
Uthibitisho wa Anwani ya Familia	Mkataba wa kukodisha au bili ya huduma ya hivi karibuni
Kitambulisho cha Mzazi au Mlezi	Leseni ya Udereva au kitambulisho cha ubalozi kutoka Marekani au nchi ya awali.

- Ikiwa huna hati zote, JCPS bado itamsajili na kumwandikisha mwanafunzi wako. Utahitajika kuwasilisha hati zako haraka iwezekanavyo.
- Ikiwa mtu mzima hana ulezi kisheria kwa watoto aliye chini ya uangalizi wake, anaweza kutumia mamlaka ya wakili au hati ya kiapo ya mlezi.
- Unaweza kuwasajili watoto wako shuleni hata kama huna makazi ya kudumu. Piga simu kwa Ofisi ya Ufikiaji na Fursa ya JCPS kupitia (502) 485-3650 upate msaada.